UZEMBE

Mwananchi Jumatatu Julai 28, 2025 Pg 3

# Madereva wahimizwa umakini, miili sita ya wanafunzi ikiagwa

**Saddam Sadick na Hawa Mathias**, Mwananchi

**Mbeya.** Vilio na simanzi vimetawala katika Shule ya Sekondari Chalangwa, wilayani Chunya mkoani Mbeya, wakati wa kuagwa kwa miili ya wanafunzi sita waliopoteza maisha katika ajali ya basi, walipokuwa wakifanya mazoezi ya utimamu wa mwili.

Wanafunzi hao wa Shule ya Sekondari Chalangwa walifariki dunia juzi saa 11:30 alfajiri baada ya kugongwa na basi la Kampuni ya Safina wakiwa wanafanya mazoezi ya kukimbia mchakamchaka na mwalimu wao katika Kijiji cha Itumba, Kata ya Chalangwa pembezoni mwa barabara ya Chunya-Mbeya.

> "Eneo la ajali lilikuwa na alama za onyo, dereva alipaswa kuwa makini. Ukaguzi wa mabasi usisubiri ajali; ufanyike kwa kushtukiza ili kubaini madereva wasio na sifaa."
>
> Ndomba Ndomba

Katika ajali hiyo wanafunzi watano walifariki dunia papo hapo na mmoja akipatiwa matibabu, huku tisa wakijeruhiwa.

Leo shule hiyo imegeuka uwanja wa majonzi wakati wa ibada ya kuwaaga marehemu hao huku viongozi wa Serikali na wananchi wakitoa pole na ushauri kuhusu usalama barabarani.

Wanafunzi waliopoteza maisha katika ajali hiyo ni Seleman Msekwa, Kenedy Masoud , Samwel Zambi, Kelvin Mwasamba, Hosea Mbwilo na Amina Ulaya. Waliopata majeraha ni Benard Mashaka, Lilian Raymond, Vicent Baraka Malema, Siwema Nasibi Simbilo, Alex Peter, Dethani Charles, Getruda Mwakyoma na Farida Mwasongole.

Serikali imetangaza kugharamia mazishi ya wanafunzi hao na kugharimia matibabu ya majeruhi wote.

Pia imetoa agizo la kusitishwa kwa mazoezi ya 'jogging' barabarani kwa wanafunzi na vikundi vya michezo, ikiwa ni tahadhari ya kuzuia ajali kama hiyo.

Kati ya walioguswa na msiba huo ni baba mlezi wa mmoja wa marehemu, Kedron Mbwilo aliyempoteza mtoto wake wa kidato cha tatu. "Ni pigo kubwa kwa familia yetu kumpoteza mtoto ambaye tulimtegemea kwa maisha ya baadaye. Tunaishukuru Serikali kwa kuungana nasi katika wakati huu mgumu," alisema kwa huzuni mzazi huyo.

Akizungumza msibani hapo, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mbaraka Batenga alitoa wito kwa waendeshaji wa vyombo vya moto kuheshimu sheria za usalama barabarani na kuwa makini katika matumizi ya barabara.

"Uzembe wa madereva umekuwa chanzo kikuu cha ajali. Madereva wafahamu kuwa vyombo wanavyoendesha vinabeba uhai wa watu, wanapaswa kuwa makini sana," alisema Batenga.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi (Taboa), Adam Mwakamalisya alieleza masikitiko yake kuhusu ajali hiyo huku akisema tayari walishapokea malalamiko dhidi ya basi hilo.

"Basi hili tayari lilishaligonga gari la halmashauri siku za nyuma. Sasa limetokea tukio hili la kusikitisha. Tushirikiane kumtafuta dereva huyo ili achukuliwe hatua za kisheria," alisema Mwakamalisya.

Wananchi pia walizungumzia ajali hiyo na kuitaka Serikali na Jeshi la Polisi upande wa usalama barabarani, kuchukua hatua kali zaidi kwa madereva wanaosababisha ajali barabarani.

Akizungumzia hilo mkazi wa Chunya, Geoffrey Mwankenja aliwataka madereva kuwa makini kabla ya kuyapita magari mengine hasa maeneo ya makazi ya watu.

"Ajali nyingi hutokea kwa uzembe wa madereva, Serikali ifuatilie kwa ukaribu," alisisitiza mwananchi huyo.

Naye Ndomba Ndomba, mkazi wa Matundasi aliliomba Jeshi la Polisi kuendelea kufanya ukaguzi wa mabasi mara kwa mara.

"Eneo la ajali lilikuwa na alama za onyo, dereva alipaswa kuwa makini. Ukaguzi wa mabasi usisubiri ajali; ufanyike kwa kushtukiza ili kubaini madereva wasio na sifa," alisisitiza.

Tukio hili limeacha majonzi si tu kwa familia za wanafunzi hao, bali kwa jamii nzima ya Chalangwa na Taifa kwa ujumla, huku wito ukiendelea kutolewa kwa wadau wote kuimarisha usalama wa barabarani na kulinda maisha ya Watanzania.

CamScanner

# Wadau watoa neno ujio mabasi ya mwendokasi

**Na REHEMA MAIGALA**

WADAU wa usafiri wamesema ujio wa mabasi yaendayo haraka katika Jiji la Dar es Salaam, utaimarisha uchumi wa Taifa na mtu mmoja mmoja.

Walisema hatua hiyo itafungua ukurasa kwa watendaji wa sekta mbalimbali kufika kwa wakati mwafaka sehemu zao za kazi.

Pia, wadau hao walisema wanafunzi watafika shuleni kwa wakati jambo ambalo litaongeza ufanisi katika masomo yao.

Akizungumza na gazeti hili mwishoni mwa wiki, Mchumi wa Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Dk. Silvester Rugeiyham alisema mabasi hayo yatapunguza changamoto iliyopo hivi sasa ya usafiri hususani asubuhi na jioni.

Hata hivyo, Dk. Rugeiyham alishauri serikali iyasimamie mabasi hayo kibiashara kupata faida na kutoa huduma ya uhakika kwa wananchi.

"Usafiri huu ukiimarishwa kibiashara faida itaonekana na itaweza kununua mabasi mengi na hatua hiyo itasaidia kuondoa changamoto ya kuwepo mabasi mabovu kama ilivyo sasa,"alisema.

Vilevile, Dk. Rugeihyamu aliitaka Kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka (UDART), kupanga utaratibu mzuri wa kupeleka mabasi hayo vituoni kuondoa msongamano mkubwa wa abiria hasa asubuhi na jioni.

Kwa upande wake Katibu Mtendaji Baraza la la Udhibiti wa Usafiri Ardhini ( LATRA CCC) Daudi Daud alisema sekta ya usafiri itarahisishwa baada ya serikali kuboresha na kujenga barabara za mwendo kasi katika njia zote za jijini, Dar es Salaam.

"Tunachowaomba wananchi wanaotumia usafiri huo wafuate sheria zilizowekwa na usafiri huo,"alisema.

Juzi, Mkuu wa Mkoa wa Daer es Salaam, Albert Charamila alifanya ziara ya kushitukiza katika kituo kikuu cha mabasi hayo Kimara na kushuhudia msongamano mkubwa wa abiria kituoni.

Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) Dk. Athumani Kihamia alisema hadi kufikia Agosti, mwaka huu mabasi 99 kati ya 101 yatawasili nchini hivi karibuni.

**USAFIRISHAJI**

**DART**

Hadi kufikia Agosti, mwaka huu mabasi 99 kati ya 101 yatawasili nchini hivi karibuni kuanza kutoa huduma kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam.

CamScanner